JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

SHULE YA SEKONDARI PROFESA PALAMAGAMBA KABUDI
S.L.P. 1568 KILOSA-MOROGORO.
Barua pepe:*profesapalamagambakabudi.secondary@kilosadc.go.tz*

**KUMB:NO.KDC/PPKSS/F5./2025/0031**

**Namba za Simu 0684-016322**

**Mkuu wa Shule 0658-240086**

**Makamu Mkuu wa 0767-070724**

**Matron/Patron 0753-321004/0786-856711**

**Tarehe .26.04.2025.**

MZAZIA /MLEZI WA MWANAFUNZI ...........................................................................

S. L. P. .......

**.......................**

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PROFESA PALAMAGAMBA KABUDI KIDATO CHA TANO MWAKA MWAKA WA MASOMO 2025/2026.**

## 1.0 UTANGULIZI.

- ✓ Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga **Kidato cha Tano** katika Shule ya Sekondari Profesa Palamagamba kabudi, **Mwaka wa Masomo 2025/2026**.
  - i) Shule hii ipo Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilosa, Tarafa ya **Magole,** Kata ya **Berega** kijiji cha **Berega,** Kitongoji cha **Gongoni.**
  - ii) Shule hii pia inapatikana kando kando ya Barabara kuu iendayo Jijini Dodoma ikitokea Mkoa wa Morogoro umbali wa kilomita 100 kutoka stendi kuu ya Mkoa wa Morogoro(Msamvu Bus Terminal).

- ✓ Ukitaka kufika shuleni fatilia maelekezo yafuatayo:-

Ukiwa unatokea Morogoro, fika stendi ya Msamvu Morogoro mjini panda gari ziendazo Gairo, shuka eneo lanjia panda (Kiegea) ya kwenda Berega mission hospital, kutoka njia

i) panda hadi shuleni pana umbali wa Kilometa moja (**01Km**) na nusu (**500M**) na usafiri wa pikipiki ni **Tshs. 1000/=** tu.

ii) Ukiwa unatokea Kilosa Makao Makuu ya Wilaya, Shule ipo umbali wa kilomita 125, utapanda gari ziendazo Dodoma,shuka eneo la njia panda (Kiegea) ya kwenda Berega mission hospital, kutoka njia panda hadi shuleni pana umbali wa Kilometa moja (**01Km**) na nusu (**500M**) na usafiri wa pikipiki ni **Tshs. 1000/=** tu.

iii) Kwa magari yanayotoka Kilosa kwenda Morogoro utashuka eneo linaloitwa Dumila, utapanda gari zinazokwenda Gairo, shuka eneo la njia panda (Kiegea) ya kwenda Berega mission hospital, kutoka njia panda hadi shuleni pana umbali wa Kilometa moja (**01Km**) na nusu (**500M**) na usafiri wa pikipiki ni **Tshs. 1000/=** tu.

- ✓ Kwa wanafunzi wanaotokea mikoa ya kanda ya ziwa, magharibi na kati kupitia Dodoma kuelekea Morogoro, shuka eneo la njia panda (Kiegea) ya kwenda Berega mission hospital, kutoka njia panda hadi shuleni pana umbali wa Kilometa moja (**01Km**) na nusu (**500M**) na usafiri wa pikipiki ni **Tshs. 1000/=** tu.

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 2.1 Sare za Shule.

i) **Wakati wa Darasani(Muda wa Vipindi);**

- ✓ Surualirangi ya Dark Blue Stimu (Grade I) mbili (02) pana (Taniapu Inch 15 hadi 16), marinda manne madogo mbele (kushoto mawili na kulia mawili), mifuko yake (miwili ya mbele ya kawaida kushoto mmoja na kulia mmoja na nyuma mmoja upande wa kulia).
- ✓ Shati mbili (02) nyeupe za tetron mikono mirefu aina ya tomato yenye mfuko mmoja yasiyobana na liwe na alama ya kidato cha tano(**V**) begani upande wa kulia.
- ✓ Soksi nyeupe saizi ya kati zisizo na pambo lolote na viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba viwe na kisigino kifupi.
- ✓ Sweta rangi ya Dark Blue.

**ii) Baada ya muda wa Darasani(Vipindi kuisha/Shamba Dress);**

- ✓ Surualirangi ya Damu ya Mzee (Redish Brown) mbili (02) pana (Taniapu Inch 15 hadi 16), marinda manne madogo mbele (kushoto mawili na kulia mawili), mifuko yake (miwili ya mbele ya kawaida kushoto mmoja na kulia mmoja na nyuma mmoja upande wa kulia).
- ✓ T-shirts moja (01) Ya njano maarufu kama form six isiyo na maandishi yoyote za kushindia.(shamba dress)
- ✓ Raba au viatu vya wazi (Open shoes).

**iii) Sare za Michezo ni:-**

- ✓ Tisheti ya Kijani, Kaptura au Bukta ya Kijani (Jezi)
- ✓ Track suit za Dark Blue,
- ✓ Soksi za michezo rangi nyeusi
- ✓ Raba/viatu vya michezo.

**iv) Sare zingine zinaruhusiwa kuvaliwa shuleni ni pamoja na;-**

- ✓ Fulana nyeupe ya ndani mbili au zaidi(Vesti)
- ✓ Nguo za ndani (chupi) dazani 1 au zaidi
- ✓ Leso (handkerchief)
- ✓ Viatu vya wazi vya kuogea(Ndala)

Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

i. Nguo za kushindia (*shamba dress*) damu ya mzee;

ii. Tai moja (*dark blue*);

iii. Tisheti (T-shirt)(***dark blue***);huratibiwa na idara ya malezi na nidhamu kupitia kwa mtoa huduma kwa gharama ya **TSH 10,000**./=ikiwa na jina la Shule na nembo yake.

IV. Traki suti daki bluu zenye ufito mweupe.Pia kwa atakayependa kununulia shuleni zinapatikana kwa gharama ya Tsh 22000/=

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10(*counterbook Quire 3*);

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);

iv. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni futi mbili na nusu (2.5)

v. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*shukalight blue na foronya zake);*

vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
x. Faili moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za taarifa zake shuleni, pia yanapatikana karibu na shuleni kwa gharama ya Tsh 3000/=.kwa atakayependa kununulia huku.
xi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
xii. Hati ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne (result slip)

**2.3 Michango mbalimbali ilipwe kupitia akaunti namba 21810031908 NMB**
**Jina la akaunti:Berega secondary school capitation account**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- ✓ Muhula wa masomo unaanza **tarehe 08/07/2025**. Kuripoti shuleni ni kuanziatarehe 0**8/07/2025** na siku ya mwisho ya kuripoti itakuwa tarehe **29/08/2025**.

**v) Sare zingine zinaruhusiwa kuvaliwa shuleni ni pamoja na;-**
- ✓ Fulana nyeupe ya ndani mbili au zaidi(Vesti)
- ✓ Nguo za ndani (chupi) dazani 1 au zaidi
- ✓ Leso (handkerchief)
- ✓ Viatu vya wazi vya kuogea(Ndal











**Sare ya darasani, sare baada ya vipindi, sare ya siku ya jumatano na ijumaa pamoja na sare ya michezo.**

**1.1 VIFAA VYA DARASANI**

**2.0 VIFAA VYA DARASANI.**

- ✓ Daftari aina ya Counter Book kumi na Sita(16) kwa ajili ya Darasani na Daftari kubwa za kawaida (msomi) kumi na Sita (16) kwa ajili ya mazoezi.

- ✓ Kalamu za wino za kutosha
- ✓ Penseli, Kifutio,pamoja na rula
- ✓ Taa ya jua (Solar) kwa ajili ya dharula ikiwa umeme utakatika.

## 2.1 VITABU VYA ZIADA

### 2.1.1 KISWAHILI.

- ✓ Nadharia ya Lugha Kiswahili 1, Kidato cha 5&6.
- ✓ Sarufi na Fasihi – Sekondari na Vyuo. Dar –es- Salaam, Tanzania Publishing House- Nkwera F. 1987
- ✓ Fasihi ya Kiswahili – Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Mulokozi M. 1996.
- ✓ Ushairi: Nadharia na Tahakiki Dar – DUP, Senkoro F. 1988.
- ✓ Kiswahili Sekondari Kidato cha Tano – T.E.T – 2016.
- ✓ Kamusi ya Kiswahili Sanifu.
- ✓ Sarufi miundo ya kiswahili sanifu- SAMIKISA.
- ✓ Sarufi maumbo ya kiswahili sanifu – SAMIKISA.

**RIWAYA.**

- ✓ Mfadhili.............................Hussein Tuwa
- ✓ Kufikirika.........................Shaban Robert
- ✓ Vuta N'kuvute---------Shafi Adam Shafi
- ✓ Usiku utakapokwisha.—Mbunda Msokile

**TAMTHILIYA.**

Kivuli kinaishi................Ibrahim Hussein
Nguzo Mama................Emmanuel Mbogo
Morani.......................Said Mohamed
Kwenye ukingo wa Thimu........Ibrahimu Hussein

**USHAIRI.**

Kimbunga...................Haji G.Haji
Chungu Tamu............Theobald Mvungi
Fungate ya uhuru...........Mohamed S.Khatibu
Mapenzi Bora

### 2.1.2 ENGLISH LANGUAGE 1&2

- ✓ Dictionary moja ya Kiingereza- Kiswahili (English – Swahili Dictionary)
- ✓ Dictionary moja ya Kiingereza- Kiingereza(English – English Dictionary)
- ✓ Advanced level English Language Structure & Sylististics(ENGLISH LANGUAGE 1)
- ✓ Ashel,N(2009)Advanced level English ,a practical Approach-DSM

- ✓ English Language for Advanced level –TIE
- ✓ Kadeghe,Michael(2011) the real English textbook for Advanced level.
- ✓ Ashel,N,(2011) Advanced level literature
- ✓ Advanced literature(2008) Nyambari Nyangwine publishers,DSM
- ✓ Achebe,A,(1966) A man of the people
- ✓ Ayi kwei Armah(1968),The beautiful ones Are Not Yet Born
- ✓ Ibsen,H,(1982) AN Enemy Of the People
- ✓ Imbuga,Fc(1976)Betrayal in the city
- ✓ Mirii Ngugi &Thing'ol(1982) I Will Marry When I Want.
- ✓ Mloka C,(2007) The Wonderful Sureon
- ✓ T.I.E. Selected poems

2.1.3 **HISTORY**

- ✓ Essentials in Advanced Level History paper 1.
- ✓ Advanced History 1 form 5 by T.I.E.

### 2.1.4 GENERALSTUDIES

- ✓ Richard r.f mbalache (2011) General Studies for advanced level certificate, f.5 1st edition b.3/2014.

Jonas Bigirwamungu& Sospeter Deogratius(2019) General studies for Advanced level

### 1.2.5. GEOGRAPHY

**(Colins Buckle)** LAND FORMS IN AFRICA

(CR.KOTHARI) RESEARCH METHODOLOGY

(H.C.THURAN) A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS

(Gohcheng.Gilian C.Morgan)HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY

(DAVID WAUGH) GEOGRAPHY AND INTERGRATED APPROACH

(JOHN.M.PRICHARD) PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA

(R.B.BUNETTE) PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAM FOR AFRICA

(G.MORGAN) HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY

(T.I.E) HUMAN GEOGRAPHY,PRACTICAL GEOGRAPHY,PHYSICAL GEOGRAPHY FOR A-LEVEL.

## 3.0. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake**

**au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu**

**wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0684-016322/0658-240086**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0767-070724**
**Mwandamizi Taaluma 0768-362557**
- **Mwandamizi Malezi 0767-070724**

### 2.2 Sheria za Madarasani

✓ Ukiukaji wa sheria hizi utasababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali:-

**i.** kelele za aina yoyote haziruhusiwi darasani. Kumbuka darasani ni mahali pa kujifunzia, sio pa kupiga kelele.

**ii.** Ni lazima kila mwanafunzi akae darasani kwa kufuata mpango uliowekwa, kutofanya hivyo ni kukiuka sheria.

**iii.** Hakuna mwanafunzi atakayetoka nje ya darasa wakati wa vipindi bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.

**iv.** Ni marufuku kuingia na chakula/kinywaji darasani au kula darasani.

**v.** Ni marufuku mwanafunzi yeyote kuandika maandishi yoyote kwenye dawati, kiti, meza, sakafu, kuta au paa za darasa/ofisi Adhabu kali itatolewa kwa atakayebainika kufanya hivyo.

**"Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na nadhifu muda wote awapo shuleni, avae sare ya shule inavyo stahili na ni marufuku kuvaa mlegezo."**

**3.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na mwanafunzi shuleni ni pamoja na;**

(a) **Medical Examination Form**,

Hii ni fomu ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule utapokua unarepoti shuleni.

(b) **Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi/Mkataba**

Hii ni fomu maalumu ya maelezo ambayo itasimulia historia ya mwanafunzi kwa ufupi hasa vipengele muhimu vinavyohitaji uangalizi wa karibu na kuahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Fomu hii pia pia utaikabidhi ofisini kwa mkuu wa shule utakapo ripoti.

(c) **Tamko la mzazi /mlezi kukiri kukubaliana na sheria za shule**

Fomu hii ni tamko maalumu la mzazi kuahidi kushirikiana na shule katika kumuwezesha mwanafunzi kusoma bila vikwazo.

(d) **Fomu ya Taarifa binafsi za Mzazi/Mlezi kuhusu Mwanafunzi,**

Hii ni fomu maalumu kwa ajili ya taarifa za usajili wa Mwanafunzi shuleni. Hivyo ijazwe kikamilifu na kwa usahihi mkubwa.(ijazwe na mzazi)

**4.0 Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kujadiliana na mwanao juu ya utayari wake katika kuzingatia yaliyo tajwa kwenye fomu hii na kuyatekelezakikamilifu**

*karibu sana shule ya sekondari profesa palamagamba kabudi.*

*"elimu kwa maarifa ongozi"*

Ngamba M. Manegese

Mkuu wa Shule

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
SHULE YA SEKONDARI PROF.PALAMAGAMBA KABUDI

**KUMB:NO.KDC/PPSS/2025/ 0031.**

## Yah: HATI YA UTII NA SHERIA ZA SHULE.

### SEHEMU "A": (IJAZWE NA MWANAFUNZI)

Mimi ..........................................................................................................................

Nimesoma nakuelewa kabisa masharti yote na sheria za shule ninazikubali sheria hizo na nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa ninaelimishwa na umma kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

Sahihi ya Mwanafunzi ............................................................ Tarehe .......................................

### SEHEMU "B": (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

Mimi ...........................................................................................................................

Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Ninathibitisha kuwa mwanangu amesoma na kuzielewa sheria za shule. Ninaahidi kuwa nitashirikiiana na uongozi wa shule kuona kuwa mwanangu anafuata taratibu zote za shule kwa manufaa yake na kwa manufaa ya umma.

Pia ninaahidi nitamuhimiza ahudhurie shule pamoja na kusoma kwa bidii maendeleo ya mwanangu.

### SEHEMU "C": NDUGU WANAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI

| NA. | JINA KAMILI LA NDUGU | UHUSIANO NA MWANAFUNZI | NAMBA YA SIMU INAYOPATIKANA MUDA WOTE |
|---|---|---|---|
| 01. | | | |
| 02. | | | |
| 03. | | | |
| 04. | | | |
| 05. | | | |

Anuani ya mzazi/mlezi.

..........................................................................

..........................................................................

Simu: ..................................................................................

Saini ..................................................................Tarehe................

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KILOSA DISTRICT COUNCIL
PROF. PALAMAGAMBA KABUDISECONDARY SCHOOL

**KUMB:NO.KDC/PPSS/2023/ 0032.**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

**FROM**: The Medical Officer
Government Hospital
............................................
............................................
............................................

Re: **MEDICAL CERTIFICATE.**

**(TO BE COMPLITED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined ........................................................................... who aspires to join form one in a year 2023 in your school as follows:

| S/No. | AREA | REMARKS |
|---|---|---|
| 01. | Skin | |
| 02. | Eyes | |
| 03. | Ears | |
| 04. | Teeth | |
| 05. | Chest | |
| 06. | Spleen | |
| 07. | Abdomen | |
| 08. | Urine | |
| 09. | Tool | |
| 10. | Hb Haemoglobin | |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Sickle Cell | |
| 12. | Asthma | |
| 13. | Pregnancy for Girls | |
| 14. | Any other Comments | |

I consider that he/she is physically not physically fit to join your school due to ........................................

....................................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................................

Signature: ............................................... Date: ................................ Official Stamp: ............................

**KUMB:NO.KDC/BSS/2023/ 0034.**

**Weka pichaya surayakoyarangihapa(Mwanafunzi)**

Yah: **HATI YA TAARIFA ZA USAJILI WA MWANAFUNZI.**

| Na. | Taarifa zinazohitajika | Taarifa zinazohitajika zijazwe hapa |
|---|---|---|
| 01. | Jina la Mzazi/Mlezi | |
| 02. | Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi | |
| 03. | Hali ya Mzazi/Mlezi | |
| 04. | Jinsia | |
| 05. | Uhusiano na Mwanafunzi | |
| 06. | E-mail ya Mzazi/Mlezi | |
| 07. | Namba ya NIDA | |
| 08. | Kazi ya Mzazi/Mlezi | |
| 09. | Anwani ya Mzazi/Mlezi | |
| 10. | Mahali unapoishi | |
| 11. | Kiwango cha Elimu | |
| 12. | Umbali (Mkoa) unapoishi kutoka shule ilipo | |
| 13. | Uraia wa Mwanafunzi | |
| 14. | Ulemavu (Haoni, Uono hafifu, Utindio wa Ubongo) | |
| 15. | Hali ya Mwanafunzi kiafya | |

Mimi ………………………………………………………………….. Mzazi/Mlezi nathibitisha/ nakiri kuwa taarifa nilizojaza kwenye jedwali hapo juu ni sahihi kabisa na endapo nikiwa nimedanganya nishitakiwe kwa mujibu wa sheria.

Sahihi: ..................................................Tarehe.............................